TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 4019, DODOMA
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978
Barua Pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

30 Aprili, 2025

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Tamko la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei 1, 2025**

Tarehe 1 Mei kila mwaka ni Siku ya Kimataifa ya Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani. Maadhimisho haya yamelenga katika kutambua mchango wa wafanyakazi duniani kote katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi kwa mwaka 2025 nchini yanaongozwa na kauli mbiu isemayo: ***"Uchaguzi Mkuu 2025 Utuletee Viongozi Wanaojali Haki na Maslahi ya Wafanyakazi, Sote Tushiriki"***

Kauli mbiu hii inawahamasisha Wafanyakazi kujitokeza kushiriki katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka huu 2025 ili kuhakikisha kwamba pamoja na wananchi wengine wanawachagua viongozi wenye kuheshimu na kulinda haki za binadamu na kusimamia misingi ya utawala bora wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

THBUB inawakumbusha wafanyakazi kuwa upatikanaji wa viongozi waadilifu utapunguza malalamiko ya wafanyakazi hasa katika masuala yanayohusu maslahi yao binafsi.

Wakati maadhimisho haya yakifanyika, THBUB inatambua na kupongeza juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika

kuhakikisha nchi inapata viongozi waadilifu, wasio na ubaguzi, wenye uzalendo na wanaozingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuendelea kuijenga Tanzania yenye amani na utulivu.

THBUB inapenda kuwakumbusha waajiri kote nchini kuhusu umuhimu wa kuzingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kazi kwa wafanyakazi walio chini yao ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira yao ya kazi; kuwashirikisha katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia mipango ya taasisi; kuepuka ubaguzi, matumizi ya lugha chafu, ukaripiaji na udhalilishaji wa kijinsia.

Nitoe rai kwa Serikali na Waajiri wote nchini kuendelea kuweka mazingira bora ya kazi na kusimamia vyema maslahi ya wafanyakazi kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Ajira ili kujenga mazingira rafiki kwa wafanyakazi kufurahia haki yao ya kufanya kazi na pia kuleta tija na ufanisi katika utendaji.

Napenda pia kutoa rai kwa kila mfanyakazi kutimiza wajibu wake kwa kufanya kazi kwa kujituma na uadilifu huku wakifuata sheria na miongozo iliyowekwa katika ajira. Tukifanya hivyo tutaleta maendeleo nchini.

Imetolewa na:

Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)
**MWENYEKITI**
**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**